

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA CHEMBA
(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wilaya)



Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. CDC/I 20/2VOL1/60

31/07/2023

**YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA KWA MKATABA
KATIKA VITUO VYA AFYA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba anakaribisha maombi ya kazi za kujitolea kutoka kwa watazania wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi ya Msaidizi wa Hesabu.

MSAIDIZI WA HESABU DARAJA LA II- NAFASI (5)

SIFA ZA MWOMBAJI.

- (i) Awe amefaulu kidato cha Nne (iv)
- (ii) Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada (Cheti) NTA level 5 ya Uhasibu kutoka Chuo kinachotambuli wa na Serikali au cheti cha ATEC I kinachotolewa na NBAA au sifa nyingine zinazolingana na hizo zinazotambulika na NBAA.

MAJUKUMU YA KAZI.

- (i) Kusimamia makusanyo ya Kituo cha Afya husika na Zahanati zinazozunguka
- (ii) Kuandika na kutunza "register" zinazohusu shughuli za uhasibu.
- (iii) Kutunza kumbukumbu za hesabu.
- (iv) Kupeleka barua/nyaraka za uhasibu Benki.
- (v) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi.

MSHAHARA.

Kwa kuzingatia ngazi ya mshahara ya Serikali TGS B₁ kwa mwezi Tsh.450,000/=

MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI TAJWA


- i. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45.
- ii. Waombaji waambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wakuaminika.
- iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kidato cha nne na sita waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika pamoja na nakala ya kitambulisho cha Uraia (Nida).

Viambatanisho hivyo vibanwe sawasawa kuondoa uwezekano wa kudondoka au kupotea. (Passport size) ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.

- v. Testimonials, "Provisional results", statement of results ", hati ya matokeo ya kidato cha Nne na Sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.
- vi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU na NECTA).
- vii. Waombaji waliostaafishwa/kupunguzwa kazi au kufukuzwa kazi katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- viii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- ix. Maombi yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza.
- x. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 13/08/2023 saa 9.30 ALASIRI na yatumwe katika anuani ifuatayo:

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA
S.L.P 830
CHEMBA – DODOMA

Imetolewa na:-


Siwema H. Jumaa
Mkurugenzi Mtendaji (W)
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
CHEMBA

Nakala: Katibu,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
Jengo la Utumishi (UDOM)
Eneo La Dkt Asha Rose Migiro,
Sanduku la posta 2320,
DODOMA.

Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Chemba
www.chembadc.go.tz

Mbao za matangazo.